# CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO TANESCO

**KUTOKA KWA: MWENYEKITI**

**KWENDA KWA: WANACHAMA WOTE**

**KUM: TS/AGM/2026/02**

**TAREHE : 10.08.2026**

**YAH: MIKUTANO YA DONDOO NA UCHAGUZI MATAWINI**

Chama kinawatangazia Wanachama wote kuwa, kinatarajia kuanza kufanya Mikutano ya Dondoo za Mkutano Mkuu wa mwaka 2026 na kuchagua wawakilishi katika matawi yake nchi nzima kuanzia tarehe 22.08.2026 kutekeleza dhana ya ushirikishwaji wa wanachama katika mipango ya Chama.

Agenda za Mkutano;

i. Elimu ya Uanachama na Bidhaa za Chama:
   - Kusajili Wanachama watoto
   - Bidhaa za Bima

ii. Hisa za JENGO

iii. Dondoo

iv. Uchaguzi wa WAWAKILISHI WA TAWI

v. Taarifa: Ugawaji wa Vyeti vya HISA na kadi za FOSA zilizokwisha muda.

**TANBIHI:**

1. Marekebisho ya Miongozo ya uendeshaji wa vyama vya Ushirika, sasa unatambua mtoto (chini ya miaka 18) kujiunga na Chama cha Ushirika kwa masharti maalum. Hivyo tunahamasisha WANACHAMA WETU WOTE KUWASAJILI WATOTO WENU KUWA WANACHAMA.

2. Afisa wa Chama atakuwepo siku moja kabla ya siku ya Mkutano kwa ajili ya kuendesha *clinic* ya huduma za Chama, na kutatua changamoto za wanachama.

3. Usajili wa rejesta ya maudhurio na uchaguzi wa Mwakilishi utafanyika KIDIJITALI na rejesta itafungwa dakika 45 baada ya Mkutano kuanza.

4. Fedha za maandalizi zitatumwa kwa Mwenyekiti/Katibu wa tawi.

Andrea Hilary, Katibu wa Bodi